# GAZETI RASMI LA SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR

*(Hupigwa Chapa kwa Amri ya Serikali)*

**Sehemu ya CXXXIV Nam. 7353** **13 Juni, 2025** **Bei Shs 4,000/=**

*Imekubaliwa na Mkuu wa Posta kuwa ni Gazeti* *Hutolewa kila Ijumaa*


**YALIYOMO** **UK**


Sheria ya Huduma Ndogo Ndogo za Fedha Zanzibar Nam.9 ya 2023
Kanuni za Huduma Ndogo Ndogo za Fedha Zanzibar (Vikundi vya Huduma Ndogo za Fedha vya Kijamii ) ........................................................................ 839


**SEHEMU YA SHERIA**

Sheria iliyotajwa hapo chini imetangazwa katika ***Gazeti Rasmi*** hili.

**Tangazo la Sheria**

Nam. 59:- Kanuni za Huduma Ndogo Ndogo za Fedha Zanzibar (Vikundi vya Huduma Ndogo za Fedha vya Kijamii )

**SHERIA YA HUDUMA NDOGO ZA FEDHA ZANZIBAR, NAM. 9 YA 2023**

**KANUNI ZA HUDUMA NDOGO ZA FEDHA ZANZIBAR (VIKUNDI VYA HUDUMA NDOGO ZA FEDHA VYA KIJAMII)**

**[Chini ya kifungu cha 61(1)]**

**MPANGILIO WA KANUNI**

**KANUNI** **MAELEZO**

**SEHEMU YA KWANZA**
**MASHARTI YA AWALI**

1. Jina fupi na kuanza kutumika.
2. Matumizi.
3. Ufafanuzi.


**Matangazo yaliyohusu maiti, kuvunjikia kwa Ushirika na baadhi ya matangazo ambayo ni muhimu kwa watu kujua yanaweza kutiwa katika Gazeti. Nakala matangazo namna hiyo, zipelekwe kwa Mhariri wa Gazeti Rasmi la Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar - Tanzania katika nyumba ya kupiga Chapa, Sanduku la Posta 261. Nakla zisichelewe kuliko Jumatatu kila wiki.**

**SEHEMU YA PILI**
**UANZISHAJI WA KIKUNDI CHA HUDUMA NDOGO ZA FEDHA CHA KIJAMII**


4. Uanzishaji wa kikundi cha huduma ndogo za fedha cha kijamii.
5. Mkutano wa awali
6. Kamati ya muda na kazi zake.
7. Mkutano wa uanzishaji na kazi zake.


**SEHEMU YA TATU**
**USAJILI WA KIKUNDI CHA HUDUMA NDOGO ZA FEDHA CHA KIJAMII**


8. Maombi ya usajili.
9. Jina la kikundi cha huduma ndogo za fedha cha kijamii.
10. Uamuzi wa maombi ya usajili.
11. Cheti cha usajili.
12. Kukataliwa kwa usajili
13. Kuhamisha cheti cha usajili
14. Kikao cha kwanza.
15. Kuomba tena usajili.
16. Daftari la kumbukumbu la vikundi vya huduma ndogo za fedha vya kijamii.
17. Kufutwa kwa usajili.


**SEHEMU YA NNE**
**UENDESHAJI**


18. Kuanza shughuli za uendeshaji.
19. Shughuli zinazoruhusiwa na zisizoruhusiwa.
20. Masharti ya uendeshaji.
21. Uwasilishaji wa taarifa.
22. Utawala wa kikundi cha huduma ndogo za fedha cha kijamii.
23. Kumlinda mlaji.
24. Mashirikiano na taasisi nyengine.
25. Ufuatiliaji wa Benki au Mamlaka Iliyokasimiwa.


**SEHEMU YA TANO**
**MASHARTI MENGINEYO**


26. Ubadilishanaji wa taarifa za mikopo.
27. Kumtumia mwalimu.
28. Kipindi cha mpito.
29. Rufaa.
30. Adhabu za jumla.
31. Hatua za kiutawala.


**JADWELI**

## SHERIA YA HUDUMA NDOGO ZA FEDHA ZANZIBAR, NAM. 9 YA 2023

## KANUNI ZA HUDUMA NDOGO ZA FEDHA ZANZIBAR (VIKUNDI VYA HUDUMA NDOGO ZA FEDHA VYA KIJAMII)

**[Chini ya kifungu cha 61(1)]**

**KWA UWEZO** niliopewa chini ya kifungu cha 61(1) cha Sheria ya Huduma Ndogo za Fedha Zanzibar, Nam.9 ya 2023, **Mimi, DKT. SAADA MKUYA SALUM**, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango, natunga Kanuni zifuatazo:

### SEHEMU YA KWANZA
### MASHARTI YA AWALI

**1**. Kanuni hizi zitajulikana kama Kanuni za Huduma Ndogo za Fedha Zanzibar (Vikundi vya Huduma Ndogo za Fedha vya Kijamii), 2025 na zitaanza kutumika baada ya kutiwa saini na Waziri na kutangazwa katika Gazeti Rasmi. Jina fupi na kuanza kutumika.

**2**. Kanuni hizi zitatumika kwa watoa huduma ndogo za fedha wa Daraja la Nne wanaofanya shughuli zao Zanzibar. Matumizi.

**3**. Katika kanuni hizi, isipokuwa kama maelezo yatahitaji vyenginevyo: Ufafanuzi.

"afisa aliyeidhinishwa" maana yake ni mtu ambaye ameteuliwa na Benki au Mamlaka Iliyokasimiwa kufanya kazi chini ya Kanuni hizi;

"Benki" ina maana kama ilivyotafsiriwa chini ya Sheria ya Benki Kuu ya Tanzania, Nam.4 ya 2006;

"Chombo cha Ubadilishanaji wa Taarifa za Mikopo" ina maana kama ilivyotafsiriwa katika Sheria;

"Daraja la Nne" maana yake ni aina ya watoa huduma ndogo za fedha inayojumuisha kikundi cha huduma ndogo za fedha cha kijamii.

"Kamati ya Muda" maana yake ni Kamati iliyochaguliwa na Mkutano wa Kwanza wa kikundi cha huduma ndogo cha kijamii ambayo itawezesha uundwaji wa kikundi;

"katiba" maana yake ni katiba iliyopitishwa na wanachama wa kikundi cha huduma ndogo za fedha cha kijamii kwa mujibu wa Kanuni hizi;

"kikundi cha huduma ndogo za fedha cha kijamii" ina maana kama ilivyotafsiriwa katika Sheria;

"Mamlaka Iliyokasimiwa" maana yake ni Mamlaka ya Serikali za Mitaa iliyokasimiwa na Benki kutekeleza kazi na uwezo wa Benki kuhusiana na vikundi vya huduma ndogo za fedha vya kijamii kwa mujibu wa Sheria;

"Mamlaka ya Serikali za Mitaa" maana yake ni kama ilivyotafsiriwa chini ya Sheria ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa, Nam.7 ya 2014;

"michango" maana yake ni makusanyo ya fedha iliyokubaliwa na wanachama;

"mtoa huduma wa huduma ndogo za fedha" inamaana kama ilivyotafsiriwa katika Sheria;

"mwanachama" maana yake ni mtu ambaye ni mwanachama kwa mujibu wa katiba ya kikundi cha huduma ndogo za fedha cha kijamii kilichosajiliwa;

"Sheria" maana yake ni Sheria ya Huduma Ndogo za Fedha Zanzibar, Nam. 9 ya 2023;

"taarifa za mikopo" maana yake ni taarifa zozote zinazojumuisha taarifa zinazohusu utambulisho wa mtu, jina kamili, tarehe ya kuzaliwa, eneo la makazi, maeneo ya makazi ya awali, hali ya ndoa, jina la mwenza, sehemu ya kazi, sehemu za awali za kazi, mwenendo wa ulipaji, madeni yaliyopo, mali na maulizo ya historia ya mikopo au taarifa zinazohusu taasisi au biashara ambazo zitasaidia kutambua taarifa za taasisi au biashara zinazohusu usajili, kodi, wakurugenzi, utawala, madeni yaliyopo, mali, maulizo ya historia ya madeni na taarifa nyengine za biashara;

"wanachama waanzilishi" maana yake ni wanachama waliohusika kuanzisha kikundi; na

"Waziri" maana yake ni kama ilivyotafsiriwa katika Sheria.

## SEHEMU YA PILI
## UANZISHAJI WA KIKUNDI CHA HUDUMA NDOGO ZA FEDHA CHA KIJAMII

Uanzishaji wa kikundi cha huduma ndogo za fedha cha kijamii.

**4**.-(1) Kikundi cha huduma ndogo za fedha cha kijamii kinaweza kuanzishwa na watu binafsi walioungana kwa lengo la kutoa huduma ndogo za fedha kwa mujibu wa masharti ya Sheria na Kanuni hizi.

(2) Bila kuathiri kanuni ndogo ya (1) ya kanuni hii, kikundi cha huduma ndogo za fedha cha kijamii kinaweza kuanzishwa na idadi ya

watu saba hadi hamsini walio na malengo yanayofanana kwa ajili ya shughuli za kikundi cha huduma ndogo za fedha cha kijamii.

**5**.-(1) Watu wanaokusudia kuanzisha kikundi cha huduma ndogo za fedha cha kijamii wataitisha mkutano wa awali kwa madhumuni ya: Mkutano wa awali.

(a) kujadili na kukubaliana kuhusu uanzishaji, malengo na katiba ya kikundi; na

(b) kuchagua kamati ya muda kwa ajili ya kuwezesha uanzishaji wa kikundi.

(2) Wajumbe wa mkutano wa awali watachukuliwa kuwa ni wanachama waanzilishi wa kikundi tarajiwa cha huduma ndogo za fedha cha kijamii.

**6**.-(1) Kamati ya muda iliyochaguliwa chini ya kanuni ya 5(1) ya Kanuni hizi itakuwa na idadi ya wajumbe kama itakavyoamuliwa kwenye mkutano wa awali. Kamati ya muda na kazi zake.

(2) Kazi za kamati ya muda zitakuwa ni:

(a) kupendekeza jina na malengo ya kikundi kinachoanzishwa;

(b) kuandaa rasimu ya katiba ya kikundi ambayo itajumuisha masuala yaliyoainishwa katika Jadweli la Kwanza la Kanuni hizi;

(c) kutoa elimu kwa wanachama watarajiwa namna ya kujiunga na kikundi cha huduma ndogo za fedha pamoja na faida zake;

(d) kuorodhesha majina ya wanachama waanzilishi na kuweka kumbukumbu za mkutano wa awali;

(e) kupendekeza muundo wa kikundi;

(f) kuandaa au kupata nyaraka zote muhimu kwa madhumuni ya kutimiza vigezo vya usajili; na

(g) kuitisha mkutano wa uanzishaji wa kikundi.

**7**.-(1) Kutakuwa na mkutano wa uanzishaji wa kikundi wa wanachama waanzilishi ambao utaandaliwa na kamati ya muda kwa madhumuni ya kuanzisha na kusajili kikundi cha huduma ndogo za fedha cha kijamii. Mkutano wa uanzishaji na kazi zake.

(2) Mkutano wa uanzishaji uliotajwa chini ya kanuni ndogo ya (1) ya kanuni hii unaweza kufanywa chini ya uongozi wa afisa aliyeidhinishwa au Mwalimu na utakuwa na kazi ya:

(a) kupitisha jina na malengo ya kikundi yaliyopendekezwa;

(b) kukubaliana kuhusu muundo wa kikundi kama ulivyopendekezwa na kamati ya muda;

(c) kupendekeza majina ya viongozi wa kikundi;

(d) kujadili na kuthibitisha rasimu ya katiba na nyaraka nyengine zilizoandaliwa na kamati ya muda kwa madhumuni ya maombi ya usajili wa kikundi; na

(e) kuipatia kamati ya muda jukumu la kukamilisha nyaraka muhimu kwa ajili ya usajili na kuziwasilisha Benki au kwa Mamlaka Iliyokasimiwa.

(3) Endapo wanachama waanzilishi au kamati ya muda imemhusisha Mwalimu kwa madhumuni ya kusaidia uanzishaji na usajili wa kikundi, majukumu ya Mwalimu yatajumuisha:

(a) kuandaa rasimu ya katiba na nyaraka nyengine muhimu kwa ajili ya uanzishaji na usajili wa kikundi;

(b) kuwapatia mafunzo wanachama waanzilishi ili kuwezesha mchakato wa uanzishaji na usajili; na

(c) kutekeleza kazi nyengine kama atakavyoelekezwa na wanachama waanzilishi au kamati ya muda kwa madhumuni ya uanzishaji na usajili wa kikundi.

(4) Majukumu ya mwalimu kwa madhumuni ya uanzishaji na usajili wa kikundi yatasita mara tu usajili wa kikundi utakapokamilika isipokuwa kama atahitajika kufanya shughuli nyengine za uhamasishaji.

## SEHEMU YA TATU
## USAJILI WA KIKUNDI CHA HUDUMA NDOGO ZA FEDHA CHA KIJAMII

Maombi ya usajili.

**8**.-(1) Kikundi cha huduma ndogo za fedha cha kijamii ambacho kinakusudia kutoa huduma ndogo za fedha kitatuma maombi ya usajili kwa Benki au kwa Mamlaka Iliyokasimiwa kwa kujaza fomu ya maombi ya usajili kama ilivyoainishwa katika Jadweli la Pili la Kanuni hizi.

(2) Maombi yaliyotajwa chini ya kanuni ndogo ya (1) ya kanuni hii yataambatanishwa na:

(a) nakala mbili za katiba zilizosainiwa na wanachama wote;

(b) nakala mbili za kumbukumbu za mikutano ya uanzishaji ambazo zimesainiwa na wanachama wote;

(c) maazimio ya wanachama ya kuanzisha na kusajili kikundi cha huduma ndogo za fedha cha kijamii kama ilivyoainishwa katika Jadweli la Tatu la Kanuni hizi;

(d) mapendekezo ya muundo wa kikundi na majina ya viongozi wanaopendekezwa na mwombaji;

(e) orodha ya wanachama, kwa kuzingatia kwamba idadi ya wanachama inakidhi kanuni ya 4(2) ya Kanuni hizi;

(f) uthibitisho wa malipo ya michango ya wanachama waanzilishi;

(g) barua ya utambulisho wa muombaji kutoka kwa Shehia; na

(h) nyaraka au taarifa nyengine yoyote muhimu kama itakavyoelekezwa na Benki au Mamlaka Iliyokasimiwa.

Jina la kikundi cha huduma ndogo za fedha cha kijamii.

**9**.-(1) Jina la kikundi cha huduma ndogo za fedha cha kijamii lililopendekezwa kwa madhumuni ya maombi ya usajili litakuwa la kipekee na litajumuisha maneno "Kikundi cha Huduma Ndogo za Fedha cha Kijamii".

(2) Bila kuathiri masharti ya kanuni ndogo ya (1) ya kanuni hii, jina la kikundi cha huduma ndogo za fedha cha kijamii halitajumuisha neno "benki".

Mazingatio ya maombi ya usajili.

**10.**-(1) Benki au Mamlaka Iliyokasimiwa, ndani ya siku kumi za kazi kutoka tarehe ya kupokea maombi ya usajili, itafanyia kazi maombi hayo na kutoa uamuzi.

(2) Endapo Benki au Mamlaka Iliyokasimiwa itapokea nyaraka ambazo hazijakamilika kwa madhumuni ya usajili, inaweza, kabla ya kuamua maombi hayo, kumtaka mwombaji:

(a) kuwasilisha nyaraka au taarifa zilizokosekana; au

(b) kurekebisha makosa ili kukidhi vigezo vya usajili.

Cheti cha usajili.

**11.**-(1) Benki au Mamlaka Iliyokasimiwa, baada ya kujiridhisha kwamba vigezo vyote vimekamilika, itasajili kikundi cha huduma ndogo za fedha cha kijamii na kukipatia cheti cha usajili kilichoainishwa katika Jadweli la Nne la Kanuni hizi.

(2) Cheti cha usajili kitaanza kutumika kuanzia tarehe iliyotolewa na kitaendelea kuwa halali hadi kitakapofutwa na Benki au Mamlaka Iliyokasimiwa.

Kukataliwa kwa usajili.

**12**.-(1) Benki au Mamlaka Iliyokasimiwa inaweza kukataa kusajili kikundi cha huduma ndogo za fedha cha kijamii kwa mujibu wa masharti ya Sheria.

(2) Endapo Benki au Mamlaka Iliyokasimiwa imekataa kusajili kikundi cha huduma ndogo za fedha cha kijamii, ndani ya siku saba kuanzia tarehe ya uamuzi huo, itatoa notisi ya maandishi kwa kikundi ikielezea sababu za kukataa.

Kuhamishwa cheti cha usajili.

**13**. Cheti cha usajili kilichotolewa chini ya Kanuni hizi hakitohamishwa kwa kikundi chengine cha kutoa huduma ndogo za fedha cha kijamii.

Kikao cha kwanza.

**14**.-(1) Kamati ya muda itaitisha kikao cha kwanza ndani ya mwezi mmoja tangu kupokea cheti cha usajili kwa madhumuni ya:

(a) kuwasilisha cheti cha usajili kwa wanachama;

(b) kuthibitisha viongozi waliopendekezwa au kuchagua viongozi wa kikundi kwa mujibu wa katiba;

(c) kuvunja kamati ya muda; na

(d) kujadili masuala mengine kama wajumbe wataona inafaa au kama ilivyoainishwa katika katiba.

(2) Mjumbe wa kamati ya muda anaweza kuchaguliwa kuwa kiongozi wa kikundi katika mkutano mkuu wa kwanza.

Kuomba tena usajili.

**15**. Kikundi cha huduma ndogo za fedha cha kijamii ambacho maombi yake ya usajili yamekataliwa chini ya kanuni ya 12 ya Kanuni hizi kinaweza kuwasilisha maombi mapya baada ya kurekebisha mapungufu yaliyoonekana wakati wa maombi ya awali au mapitio yaliyofuata yamerekebishwa au kushughulikiwa vyenginevyo.

Daftari la kumbukumbu la vikundi vya huduma ndogo za fedha vya kijamii.

**16**.-(1) Benki au Mamlaka Iliyokasimiwa itaweka na kutunza daftari la kumbukumbu la vikundi vya huduma ndogo za fedha vya kijamii.

(2) Daftari la kumbukumbu lililotajwa katika kanuni ndogo ya (1) ya kanuni hii itakuwa na taarifa zifuatazo:

(a) jina, anuani na mawasiliano ya vikundi;

(b) majina na mawasiliano ya viongozi wa kikundi;

(c) eneo la kutoa huduma;

(d) namba ya usajili;

(e) tarehe ya usajili;

(f) idadi ya wanachama; na

(g) taarifa nyengine yoyote ambayo Benki au Mamlaka Iliyokasimiwa itaona inafaa.

Kufutwa kwa usajili.

**17**.-(1) Benki au Mamlaka Iliyokasimiwa, pale itakapojiridhisha kwamba kikundi cha huduma ndogo za fedha cha kijamii kilichosajiliwa kimeshindwa kutekeleza vigezo na masharti ya usajili, au kimekiuka masharti ya Sheria au Kanuni hizi, inaweza kufuta cheti cha usajili na kuondoa jina la kikundi katika daftari la kumbukumbu.

(2) Endapo Benki au Mamlaka Iliyokasimiwa imefuta usajili wa kikundi cha huduma ndogo za fedha cha kijamii, itakipatia kikundi notisi ya maandishi ambayo pamoja na mambo mengine, itaelezea sababu za uamuzi wake.

## SEHEMU YA NNE
## UENDESHAJI

Kuanza shughuli za uendeshaji.

**18**.-(1) Kikundi cha huduma ndogo za fedha cha kijamii kilichosajiliwa kitaanza uendeshaji wake ndani ya miezi mitatu kutoka tarehe ya usajili.

(2) Benki au Mamlaka Iliyokasimiwa inaweza, ndani ya siku kumi na nne na kwa notisi ya maandishi, kufuta usajili wa kikundi cha huduma ndogo za fedha cha kijamii ambacho kimeshindwa kuanza uendeshaji wake kwa mujibu wa kanuni ndogo ya (1) ya kanuni hii.

(3) Kikundi cha huduma ndogo za fedha cha kijamii kilichofutiwa usajili chini ya kanuni ndogo (2) ya kanuni hii kinaweza kuwasilisha maombi mapya kwa mujibu wa kanuni ya 8(1) ya Kanuni hizi.

Shughuli zinazoruhusiwa na zisizoruhusiwa.

**19**.-(1) Kwa kuzingatia masharti ya Kanuni hizi, shughuli zinazoruhusiwa kufanywa na kikundi cha huduma ndogo za fedha cha kijamii zitajumuisha:

(a) kuhamasisha ukusanyaji wa michango kutoka kwa wanachama wake;

(b) kutoa mikopo kwa wanachama wake;

(c) kuhamasisha ukusanyaji wa fedha kwa ajili ya ustawi wa kijamii na kiuchumi kwa wanachama wake; na

(d) shuhuli za uwekezaji.

(2) Kikundi cha huduma ndogo za fedha cha kijamii hakiruhusiwi kujishuhulisha na:

(a) kupokea akiba kutoka kwa wasio wanachama; na

(b) kufungua tawi, wakala au kituo cha huduma.

Masharti ya uendeshaji.

**20**.-(1) Kikundi cha huduma ndogo za fedha cha kijamii kilichosajiliwa:

(a) kitakuwa na anuani ya mahali au eneo wanalokutana kutoa huduma ndogo za fedha;

(b) kitatoa huduma ndogo za fedha kwa mujibu wa Sheria, Kanuni hizi na katiba yake;

(c) kitafungua na kuendesha hesabu katika benki, taasisi fedha au aina yoyote ya hesabu kwa ajili ya kuendesha shughuli zake;

(d) kitawajibika kwa Benki au Mamlaka Iliyokasimiwa;

(e) kitagawa faida kwa wanachama wake kwa mujibu wa katiba yake;

(f) kitaweka na kutunza taarifa za kumbukumbu za msingi za fedha na taarifa nyengine muhimu zinazohusu uendeshaji wake;

(g) kitaweka na kutunza kumbukumbu za vikao, daftari la kumbukumbu la wanachama, nakala za katiba na kumbukumbu nyengine muhimu; na

(h) kitawasilisha ripoti na taarifa nyengine zozote muhimu kwa Benki au Mamlaka Iliyokasimiwa kama ilivyoainishwa katika Kanuni hizi.

(2) Benki au Mamlaka Iliyokasimiwa inaweza kutoa matoleo na miongozo kwa madhumuni ya kuwezesha utekelezaji wa masharti ya uendeshaji kwa mujibu wa kanuni ndogo ya (1) ya kanuni hii.

Uwasili-shaji wa taarifa.

**21**. Kikundi cha huduma ndogo za fedha cha kijamii kitawasilisha taarifa kwa Benki au Mamlaka Iliyokasimiwa katika muundo na namna kama itakavyoelekezwa na Benki au Mamlaka Iliyokasimiwa.

Utawala wa kikundi cha huduma ndogo za fedha cha kijamii.

**22**.-(1) Kikundi cha huduma ndogo za fedha cha kijamii kitahakikisha masuala yote yanayohusu utawala wa kikundi yameainishwa katika katiba yake.

(2) Kwa madhumuni ya kuhakikisha utawala bora, kikundi cha huduma ndogo za fedha cha kijamii:

(a) kitaitisha mikutano ikiwemo mikutano ya kawaida na mikutano mikuu kwa namna ilivyoainishwa katika katiba yake;

(b) kitachagua viongozi wenye uadilifu kwa mujibu wa katiba yake;

(c) kutahakikisha uwazi na uwajibikaji; na

(d) kitafanya shughuli nyengine yoyote kama itakavyoonekana inafaa.

Kumlinda mlaji.

**23**. Kwa madhumuni ya kuzingatia misingi ya kumlinda mlaji, kila kikundi cha huduma ndogo za fedha cha kijamii:

(a) kitakuwa na taratibu za kushughulikia malalamiko na kutatua migogoro katika katiba yake;

(b) kitakuwa na mfumo wa kutoa elimu ya kifedha kwa wanachama wake;

(c) kitahakikisha kwamba vigezo na masharti ya mikopo au huduma zinazohusu mikopo ni ya wazi, haki, yanakubalika na yanalinda haki za wanachama;

(d) kitaweka wazi ripoti na taarifa zinazohusu mwenendo wa kikundi kwa wanachama wake;

(e) kitahakikisha kwamba kila mwanachama wa kikundi anaielewa katiba;

(f) kitahakikisha kwamba taratibu za kukusanya na kurejesha madeni zinalinda haki za wanachama; na

(g) kitafanya shughuli nyengine yoyote inayokusudiwa kulinda haki na maslahi ya wanachama wake.

Mashiri-kiano na taasisi nyengine.

**24**.-(1) Kikundi cha huduma ndogo za fedha cha kijamii kinaweza kushirikiana na taasisi nyengine kwa madhumuni ya uendeshaji bora wa shughuli zake ikiwemo upatikanaji wa:

(a) huduma za kifedha kutoka benki na taasisi za fedha ikiwa ni pamoja na mikopo na hesabu za benki;

(b) misaada ya kifedha kutoka kwa asasi au taasisi zisizo za kifedha; na

(c) elimu ya fedha na huduma zingine za uwezeshaji kutoka kwa asasi au taasisi husika.

(2) Endapo kikundi cha huduma ndogo za fedha cha kijamii kinakusudia kupata mkopo kutoka kwa benki, taasisi ya fedha au taasisi nyengine yoyote, kitahakikisha kwamba:

(a) vigezo na masharti ya mkopo ni ya wazi na yanakubalika na wanachama wote; na

(b) mkopo hautazidi jumla ya mali za kikundi isipokuwa kama mkopo huo una dhamana ambayo inaweza kufidia mkopo wote.

(3) Endapo kikundi cha huduma ndogo za fedha cha kijamii kinapata huduma ya fedha kutoka benki, taasisi ya kifedha au taasisi nyengine yoyote inayotoa huduma ndogo za fedha kidigitali, kitahakikisha wanachama wake wana uelewa wa kutosha wa huduma inayotolewa ikiwemo vihatarishi, gharama na faida.

Ufuatiliaji wa Benki au Mamlaka Iliyokasi-miwa.

**25**.-(1) Benki au Mamlaka Iliyokasimiwa itafanya ufuatiliaji endelevu wa uendeshaji wa vikundi vya huduma ndogo za fedha vya kijamii.

(2) Benki au Mamlaka Iliyokasimiwa, kwa madhumuni ya ufuatiliaji wa uendeshaji wa kikundi:

(a) itapitia na kuchambua taarifa husika zilizowasilishwa na kikundi cha huduma ndogo za fedha cha kijamii;

(b) itapitia na kuchambua malalamiko na migogoro iliyowasilishwa kwa Benki au Mamlaka Iliyokasimiwa kwa madhumuni ya kuyapatia ufumbuzi;

(c) itavitembelea rasmi vikundi vya huduma ndogo za fedha vya kijamii ili kubaini utendaji kazi wake na uzingatiaji wa masharti ya Sheria na Kanuni hizi; na

(d) itatekeleza majukumu yoyote kama itakavyoona inafaa.

(3) Endapo Benki au Mamlaka Iliyokasimiwa, katika kutekeleza majukumu yake chini ya kanuni ndogo ya (2) ya kanuni hii itabaini mapungufu, inaweza, kwa maandishi kutoa ushauri au kukielekeza kikundi cha huduma ndogo za fedha cha kijamii kurekebisha mapungufu hayo ndani ya siku thelathini au kwa kipindi ambacho itaona kinafaa.

## SEHEMU YA TANO
## MASHARTI MENGINEYO

Ubadilishanaji wa taarifa za mikopo.

**26**.-(1) Kila kikundi cha huduma ndogo za fedha cha kijamii kitaweka na kutunza taarifa za mikopo za wanachama wake kwa madhumuni ya kubadilishana taarifa kupitia Chombo cha Ubadilishanaji wa Taarifa za Mikopo.

(2) Taarifa ya mikopo chini ya kanuni hii itawasilishwa kwa Chombo cha Ubadilishanaji wa Taarifa za Mikopo na kubadilishana kwa namna ambavyo itaelekezwa na Benki na kwa mujibu wa masharti ya Sheria na Sheria ya Benki Kuu ya Tanzania, Nam.5 ya 2006.

(3) Kikundi cha huduma ndogo za fedha cha kijamii kitahakikisha kwamba wanachama wote wameridhia kwa maandishi kuruhusu kikundi kupata, kubadilishana au kuweka wazi taarifa zote za mikopo zinazohusu wanachama kwa wakopeshaji au Chombo cha Ubadilishanaji wa Taarifa za Mikopo.

Kumtumia mwalimu.

**27**.-(1) Kikundi cha huduma ndogo za fedha cha kijamii kinaweza kumtumia mwalimu kwa madhumuni ya kuhamasisha shughuli za kikundi.

(2) Mwalimu atakayetumiwa chini ya kanuni ndogo ya (1) ya kanuni hii hatokuwa na haki za kipekee za kutoa huduma za uhamasishaji kwa kikundi.

Kipindi cha mpito.

**28**.-(1) Kikundi cha huduma ndogo za fedha cha kijamii ambacho kilikuwa kinafanya shughuli za huduma za fedha kabla ya kuanza kutumika kwa Kanuni hizi na ambacho kinakusudia kuendelea kutoa huduma hiyo, ndani ya miezi sita baada ya kuanza kutumika kwa Kanuni hizi, kitatakiwa kuomba usajili kwa mujibu wa masharti ya Kanuni hizi.

(2) Kikundi cha huduma ndogo za fedha cha kijamii ambacho kitashindwa kufuata masharti ya kanuni ndogo ya (1) ya kanuni hii, kitatakiwa kuacha kutoa huduma na kusita kuwa Kikundi cha huduma ndogo za fedha cha kijamii.

Rufaa.

**29**.-(1) Kikundi cha huduma ndogo za fedha cha kijamii ambacho hakijaridhika na maamuzi ya Benki au Mamlaka Iliyokasimiwa chini ya Kanuni hizi kinaweza kukata rufaa kwa Waziri, ndani ya siku thelathini, kutoka tarehe ya ya kutolewa kwa uamuzi huo.

(2) Rufaa iliyokatwa chini ya kanuni ndogo ya (1) ya kanuni hii itakuwa ya maandishi na itaelezea kwa uwazi yafuatayo:

(a) sababu za rufaa; na

(b) masuala mengine yoyote muhimu.

(3) Waziri, ndani ya siku sitini kutoka tarehe ya kupokea maombi ya rufaa, ataamua rufaa hiyo.

(4) Katika kuamua rufaa chini ya kanuni ndogo ya (3), Waziri anaweza kumtaka mkata rufaa kuwasilisha taarifa na nyaraka zozote muhimu ambazo zinajenga msingi wa rufaa yake.

Adhabu za jumla.

**30**. Mtu yeyote ambaye atakiuka masharti ya Kanuni hizi, endapo adhabu haijaainishwa atakuwa ametenda kosa na akitiwa hatiani, atalipa faini isiyopungua Shilingi Laki Tano na isiyozidi Shilingi Milioni Moja au kifungo kisichopungua miezi mitatu na kisichozidi mwaka mmoja au vyote kwa pamoja.

Hatua za kiutawala.

**31**.-(1) Bila kuathiri adhabu zilizowekwa kwenye Sheria, endapo kikundi cha huduma ndogo za fedha cha kijamii kimeshindwa kutekeleza masharti ya Sheria, Kanuni hizi au katiba yake, Benki au Mamlaka Iliyokasimiwa inaweza kuchukua hatua za kiutawala kama itakavyoona inafaa kuhakikisha utekelezwaji wa masharti hayo.

(2) Hatua za kiutawala zilizotajwa chini ya kanuni ndogo ya (1) ya kanuni hii zitajumuisha:

(a) kutoa onyo au amri ikikielekeza kikundi cha huduma ndogo za fedha cha kijamii kurekebisha mapungufu;

(b) kuwasimamisha viongozi kutekeleza majukumu yao endapo viongozi hao wamevunja masharti ya Sheria, Kanuni hizi au sheria nyingine yoyote;

(c) kusimamisha au kufuta usajili; na

(d) hatua nyengine yoyote inayokusudia kuhakikisha kuna utekelezaji wa Sheria na Kanuni hizi.

## JADWELI LA KWANZA

### VIPENGELE VYA MSINGI VYA KATIBA YA KIKUNDI CHA HUDUMA NDOGO ZA FEDHA CHA KIJAMII
**[Chini ya kanuni ya 6(2)(b)]**

Kwa mujibu wa kanuni ya 6 (2), Katiba ya kikundi cha huduma ndogo za fedha cha kijamii itajumuisha yafuatayo:

1 Jina, anuani ya mahali na mawasiliano;

2 Sehemu ya biashara na eneo la uendeshaji;

3 Dhamira, Dira na Malengo ya kikundi;

4 Taarifa za uanachama ikijumuisha, michango ya uanachama, michango ya vipindi, kukubaliwa uanachama, haki, wajibu, kusimamishwa na kufutwa uanachama;

5 Masuala ya utawala yakijumuisha uongozi, muda, uchaguzi, majukumu ya viongozi, kufutwa na kusimamishwa kwa viongozi;

6 Mikutano ikijumuisha ya Kawaida, Maalum na Mikutano ya Mwaka;

7 Taratibu za mkutano zikijumuisha notisi, ajenda, akidi, kumbukumbu za mikutano na maazimio;

8 Masuala ya uendeshaji yakijumuisha taratibu za kuhamasisha ukusanyaji wa fedha na utoaji wa mikopo;

9 Taratibu za mgawanyo wa faida;

10 Taarifa na utunzaji kumbukumbu zikijumuisha kuweka wazi taarifa za fedha na taarifa kwa wanachama na mamlaka husika kwa madhumuni ya uwazi;

11 Utaratibu wa kushughulikia malalamiko na migogoro;

12 Uvunjaji wa kikundi ikijumuisha sababu na taratibu; na

Mapitio na marekebisho ya katiba.

**JADWELI LA PILI**

---

**MAOMBI YA USAJILI WA KIKUNDI CHA HUDUMA NDOGO ZA FEDHA CHA KIJAMII**
**[Chini ya kanuni ya 8(1)]**

---

**GAVANA** **Anuani ya Mwombaji**

**BENKI KUU YA TANZANIA**

**S. L. P …………………………….**

**ZANZIBAR**

**AU**

**MKURUGENZI**
**……………………………..**

**S.L. P ……………………….**

**ZANZIBAR**

**KUH: MAOMBI YA USAJILI WA KIKUNDI CHA HUDUMA NDOGO ZA FEDHA CHA KIJAMII**

Sisi, tulioweka saini, kwa niaba ya wanachama wa kikundi cha huduma ndogo za fedha cha kijamii kinachopendekezwa, tunaomba usajili wa kikundi kiitwacho ………………………………kilichopo Shehia ya …………………………Wilaya ya…………….Mkoa wa……………………kutoa huduma ndogo za fedha kwa mujibu wa Sheria ya Huduma Ndogo za Fedha Zanzibar, 2023.

Kwa mujibu wa kanuni ya 8(2), tunaambatanisha maombi yetu pamoja na vifuatavyo:

(a) nakala mbili za katiba zilizosainiwa na wanachama wote;

(b) nakala mbili za kumbukumbu za mkutano wa awali na mkutano anzilishi wa kikundi zilizosainiwa na wanachama wote;

(c) azimio la kuanzisha kikundi cha huduma ndogo za fedha cha kijamii kama lilivyo ainishwa katika Jadweli la Pili;

(d) muundo wa kikundi uliopendekezwa na majina ya viongozi waliopendekezwa;

(e) orodha ya wanachama kama ilivyoaainishwa chini ya kanuni 4 (2);

(f) uthibitisho wa malipo wa michango ya uanachama kwa wanachama waanzilishi; na

(g) barua ya utambulisho kutoka ofisi ya Shehia.

Pia, tunatamka kwamba taarifa tulizozitoa hapo juu ikijumuisha viambatanisho ni sahihi, kwa kadri ya uelewa wetu na tunavyoamini.

| **JINA** | **SAINI** |
|---|---|
| 1. ............................................................ | ............................... |
| 2. ............................................................ | ............................... |
| 3. ............................................................. | ............................... |
| 4. ............................................................ | ............................... |
| 5. ............................................................ | .............................. |

## JADWELI LA TATU

## AZIMIO LA KUANZISHA KIKUNDI CHA HUDUMA NDOGO ZA FEDHA CHA KIJAMII

**[Chini ya kanuni ya 8(2)(c)]**

Sisi tulioweka saini hapo chini, katika mkutano uliofanyika tarehe ……/…/20………. mahali ...................... tumekubaliana na kuamua kuanzisha kikundi cha huduma ndogo za fedha cha kijamii kitachojulikana kwa jina la ………………………………KIKUNDI CHA HUDUMA NDOGO ZA FEDHA CHA KIJAMII

| JINA LA MWANACHAMA | SAINI |
|---|---|
| 1. ............................................. | ................................ |
| 2. ........................................... | ................................ |
| 3. ........................................... | ................................ |
| 4. ........................................... | ................................ |
| 5. ........................................... | ................................ |
| 6. .......................................... | ................................. |
| 7. .......................................... | ................................ |

**JADWELI LA NNE**

**BENKI KUU YA TANZANIA/MAMLAKA ILIYOKASIMIWA**

**CHETI CHA USAJILI**
**[Chini ya kanuni ya 11(1)]**

**(Nembo ya Halmashauri)**

Na. ya Usajili. ........................................

Hii ni kuthibitisha kwamba Kikundi cha Huduma Ndogo za Fedha cha Kijamii cha...................................................... kilichopo Shehia ya...........................Wilaya ya ..................................Mkoa wa.................. ........... kimesajiliwa baada ya kukidhi masharti yaliyopo chini ya kifungu cha 6 (1) cha Sheria ya Huduma Ndogo za Fedha Zanzibar, 2023.

Tarehe........................mwezi.................................

**MUHURI** **JINA NA SAINI**

**Zimetiwa** saini leo tarehe 20 Mei, 2025

**(MHE. SAADA MKUYA SALUM)**
**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS,**
**FEDHA NA MIPANGO,**
**ZANZIBAR**

LIMEPIGWA CHAPA NA WAKALA WA SERIKALI WA UCHAPAJI ZANZIBAR-2025